**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**

BRELA
BUSINESS REGISTRATIONS AND LICENSING AGENCY

## WAKALA WA USAJILI WA BIASHARA NA LESENI

# TAARIFA KWA UMMA

## UWASILISHAJI WA TAARIFA ZA UMILIKI MANUFAA KATIKA KAMPUNI

Dar es Salaam- Januari 06, 2026

Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), unapenda kuwakumbusha Wamiliki wa Kampuni zote zilizosajiliwa nchini Tanzania kutekeleza wajibu wao wa kisheria wa kuwasilisha Taarifa za Wamiliki Manufaa (Beneficial Owners – BOs) wa kampuni husika.

Kampuni yoyote iliyosajiliwa Tanzania ambayo haijawasilisha taarifa za Wamiliki Manufaa haitaruhusiwa kufanya muamala wowote na Msajili wa Kampuni hadi pale itakapokamilisha uwasilishaji wa taarifa hizo.

Miamala inayozuiwa ni pamoja na uwasilishaji wa Taarifa za Mwaka (Annual Returns), usajili wa mabadiliko ya taarifa za kampuni (change of particulars), maombi ya taarifa za hali ya kampuni (company search), usajili wa dhamana (charges), upekuzi wa nyaraka (perusal), maombi ya kurejeshewa haki za kuingia kwenye mfumo (access rights) kwa waliopoteza viingilio, pamoja na uidhinishaji wa nakala za nyaraka halisi (certification of documents).

Inasisitizwa kuwa uwasilishaji wa Taarifa za Wamiliki Manufaa ni takwa la kisheria chini ya Kifungu cha 469 cha Sheria ya Kampuni, Sura 212, toleo la mwaka 2023, pamoja na Kanuni za Umiliki Manufaa za mwaka 2023 zilizochapishwa kupitia Tangazo la Serikali Na. 714 la tarehe 22 Septemba, 2023.

Uwasilishaji wa Taarifa hizi unafanyika kupitia mfumo wa kielektroniki na maelezo ya jinsi ya kujisajili yanapatikana katika anwani https://bo.brela.go.tz/ au wasiliana nasi kupitia kituo cha huduma kwa mteja kwa namba +255 (0) 222 212 800 na anuani ya barua pepe maoni@brela.go.tz

Imetolewa na:

**Kitengo cha Mawasiliano na Uhusiano kwa Umma**